

TAARIFA YA WILAYA YA MUSOMA KWA MKUU WA MKOA WA MARA MHE. CAPT. ASERI MSANGI

1.0. UTANGULIZI:

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Kwa moyo mkunjufu sana tunakukaribisha katika Wilaya ya Musoma ikiwa ni ziara yako ya pili tangu uhamishiwe Mkoa wa Mara katika kutekeleza majukumu ya kitaifa ambayo kwetu sisi yatafungua mlango wa maendeleo zaidi. Mhe. Mkuu wa mkoa karibu sana.

Awali ya yote ninaomba upokee taarifa ya Wilaya ya Musoma ambayo inajumuisha shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wilaya.

2.0. ULINZI NA USALAMA

Hali ya Ulinzi na Usalama katika Wilaya ya Musoma kwa ujumla ni shwari. Japo bado yapo matukio madogomadogo yanayojitokeza vyombo vya ulinzi kupitia jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Wananchi wanajitahidi kudhibiti na kusimamia usalama katika maeneo yote ya Wilaya.

Kwa sasa hali ni shwari ukilinganisha na kipindi cha mwaka 2010 - 2012, hii imetokana na mikakati thabiti ya Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya, Kata na Mitaa. Mikakati mikubwa mitatu (3) iliyotumika na inayoendelea kutumika ni kama ifuatavyo:-

- (1) Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Sera ya Ulinzi na Usalama kwa kusimamia utekelezaji wa Sera ya Ulinzi shirikishi na Polisi Jamii. Sera hii inahamasisha na kutoa elimu kwa jamii ili watambue kuwa shughuli ya Ulinzi na Usalama si la Jeshi la Polisi pekee bali ni jukumu la wananchi wote.
- (2) Kuimarisha muundo wa utendaji kazi kwa Kamati za Ulinzi na Usalama kuanzia ngazi ya Mitaa na Kata.
- (3) Kuimarisha Doria jeshi la Polisi ili kudhibiti uhalifu na matukio ya vuvunjifu wa amani katika Mtaa.

Kutokana na mikakati hiyo hapo juu, ndiyo sababu kubwa ya mafanikio yanayopatikana. Wilaya inaendelea kusimamia kwa nguvu ili kuendelea kuwa na hali nzuri ya Ulinzi na Usalama katika Wilaya yetu.

Msisitizo unawekwa kwa viongozi wote kuhakikisha Mikakati hii inakuwa endelevu na kila Mtaa kunakuwa na Vikundi vya Ulinzi shirikishi Hai na vinavyofanya kazi.

3.0. MAELEZO MAFUPI YA WILAYA:

3.1. Hali ya kijiografia ya Wilaya

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa upande wa Kaskazini, Mashariki, Kusini na Kaskazini imepakana na Wilaya ya Butiama

Eneo la Halmashauri ni kilometa za mraba 63 lenye idadi ya watu wapatao 134,327 (Wanaume 62,694 na Wanawake 71,633) kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012.

3.3. Hali ya Hewa

Kuna misimu miwili ya mvua katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma. Msimu mdogo ni mvua za vuli ambazo hunyesha mwezi Septemba hadi Desemba na mvua za masika ambao ni msimu mrefu na mvua hunyesha kuanzia mwezi Februari hadi Mei. Wastani wa mvua ni mm 350. Hali ya joto ni kati ya 31.1⁰C – 31.5⁰C.

3.4. Utawala

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Eneo la Wilaya ya Musoma ambalo pia ndio eneo la Manispaa ya Musoma kuna Tarafa 1 ya Musoma Mjini. Zipo kata 16 ambazo ni Mukendo, Mwigobero, Kitaji, Iringo, Nyasho, Kamunyonge, Mwisenge, Makoko, Buhare, Nyamatare, Kigera, Kwangwa, Nyakato, Mshikamano, Rwamlimi na Bweri. Kata zote 16 zina jumla ya Mitaa 73.

3.5. Siasa

Wilaya ya Musoma ina Jimbo moja la Uchaguzi ambalo ni Musoma Mjini. Kutokana na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, Chama cha Mapinduzi kilipata viti 3 vya udiwani na Vyama vya Upinzani kwa ujumla wake vilipata viti 10 vya Udiwani. Hivyo CCM ina Madiwani 4, CUF 3 na CHADEMA 11.

Aidha kiti cha Ubunge kilichukuliwa na CHADEMA katika uchaguzi wa mwaka 2010. Hali ya kisiasa ni tulivu. Kwa sasa hakuna matatizo makubwa ambayo yanasababishwa na vyama vya siasa vilivyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.

Katika Uchaguzi wa viongozi wa mamlaka ya Serikali za mitaa uliofanyika tarehe 14/12/2014, Mitaa yote 73 na Kata zote 16 zilishiriki uchaguzi huo.

Chama cha Mapinduzi kilipata viti vya Wenyeviti wa Mitaa **42** na chama cha Demokrasia na Maendeleo kilipata viti **29** katika uchaguzi huo mitaa miwili (**2**) ya Zanzibar (Makoko) na Kitaji D (Kitaji) matokeo ya uchaguzi hayakutolewa baada ya kutokea vurugu na fujo ambazo zingepelekea kuhatarisha usalama wa wasimamizi wa uchaguzi, askari wa vituo na wananchi kwa ujumla. Marudio ya uchaguzi katika mitaa hiyo ulikuwa umepangwa kufanyika tarehe

21/12/2014 lakini ulisitishwa kwa amri ya Mahakama mpaka shauri lililowasilishwa Mahakamani litakapotolewa ufumbuzi.

4.0. HALI YA UTUMISHI

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Kwa mujibu wa ikama iliyoidhishwa mwaka wa fedha 2014/2015 ambayo ndiyo tumeendelea kuitekeleza kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Halmashauri inamahitaji ya watumishi **2,110**, hadi kufikia tarehe **31 Mei 2015**, Halmashauri ilikuwa na jumla ya watumishi wapatao **1,665**, hivyo kutokana na uhalisia wa mahitaji hayo kunaifanya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kuwa na upungufu wa watumishi **445**.

Jedwali Na. 1: Hali ya Utumishi Halmashauri ya Manispaa ya Musoma 2015/2016

Idara/Kitengo	Watumishi hitajika	Watumishi waliopo	Upungufu
Utawala	60	51	9
Fedha	29	12	17
Mipango Miji	29	9	20
Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji	5	3	2
Maendeleo ya Jamii	27	19	8
Afya Kinga na Tiba	236	179	57
Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika	29	18	11
Mifugo na Uvuvi	15	9	6
Elimu Msingi	812	777	35
Elimu Sekondari	743	520	223
Ujenzi	21	10	11
Maji	3	1	2
Ugavi na Ununuzi	7	2	5
Sheria	8	1	7
Ukaguzi wa ndani	4	2	2
Ushirika	3	2	1
TEHAMA	2	1	1
Nyuki	2	0	2
Uchaguzi	2	0	2
Watendaji wa Mitaa	73	49	24
Jumla	2,110	1,665	445

5.0. UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM (2010-2015)

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma inaendelea kutekeleza ilani ya uchaguzi ya CCM (2010-2015) kama ilivyoanishwa kwenye ibara mbalimbali kama vile Mapinduzi ya Kilimo kutekelezwa kwa ukamilifu, malengo ya mpango wa

maendeleo ya Sekta ya Kilimo na Kauli mbiu ya Kilimo kwanza (Ibara ya 33) ambapo ushauri kuhusu kanuni bora za kilimo umetolewa kwa wakulima **5,430** na pia elimu imetolewa kwa wakulima kupitia vikundi 12 vya wakulima, Vikundi 3 vimewezeshwa kuanzisha kilimo cha mazao ya bustani kwa kutumia teknolojia ya Vyama 9 vya ushirika vimeanzishwa. Nyumba, Mipango Miji, Upimaji na ramani (Ibara ya 60) ambapo michoro ya kimipango miji 9 imeandaliwa na jumla ya viwanja **1,268** vilipimwa. Aidha Halmashauri ilitoa eneo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi katika Kata ya Buhare.

Ajira (Ibara ya 22) ambapo tatizo la upungufu wa ajira limeendelea kushughulikiwa na Wilaya pamoja na wadau wake wa maendeleo. Juhudi zimefanyika kuhamasisha jamii ili kuanzisha vyama vya ushirika ambapo Halmashauri katika mapato yake imechangia Tshs. 60,000,000.00 kwa ajili ya mikopo ya vikundi vya wanawake na vijana. Vikundi vya vijana 37 na 70 vya wanawake wamenufaika na mfuko huo. Changamoto zilizojitokeza wakati wa utoaji wa mikopo ni pamoja wakopaji wengi ni wanawake na mikopo inayotolewa hupokonywa na baadhi ya wanaume, upungufu wa elimu ya ujasiriamali kwa wanavikundi na mahitaji ya wakopaji kuwa juu kuliko uwezo wa wakopeshaji.

Aidha utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM umeendelea vizuri katika ibara zingine kama vile Miundombinu ya barabara (Ibara ya 64), Uboreshaji huduma za jamii (Ibara ya 84), Utawala Bora (Ibara ya 185).

6.0. SHUGHULI ZA KIUCHUMI:

Shughuli za kiuchumi kwa wakazi wa Musoma ni pamoja na:-

- Biashara
- Kilimo
- Uvuvi
- Ufugaji

6.1 MAENDELEO YA SEKTA YA KILIMO:

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Eneo linalolimwa linakadiriwa kufikia jumla ya **hekta 650** eneo hili linajumuisha eneo ambalo bado halijaendelezwa pamoja na maeneo ya makazi. Mazao yabayolimwa ni pamoja na viazi vitamu, mahindi, mpunga, maharage, mhogo na mazao ya bustani. Ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya bustani hususan zao la nyanya Wilaya inahamasisha wakulima wa mazao ya bustani kulima kwa kutumia teknolojia ya kitalu nyumba (geen house farming).

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya (DADPS) katika mwaka wa fedha 2014/2015 Halmashauri ilitenga Tshs. **25,000,000.00** fedha iliyokusudiwa katika uwekezaji wa kilimo kwa kutumia teknolojia ya kitalu nyumba. Katika mwaka 2015/2016 Halmashauri imetengewa fedha

kiasi cha Tshs. **25,000,000.00** kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya (DADPS). Aidha mikakati ya kuongeza tija inafanyika kwa kuelimisha wakulima kulima mazao yanayostahimili ukame, kutumia mbegu bora, kuweka makinga maji, matumizi sahihi ya viuatilifu pamoja na matumizi ya mbolea.

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Hali ya upatikanaji wa mazao ya chakula (nafaka) ni ya kuridhisha katika soko la Mjini Musoma na masoko ya pembezoni. Upatikanaji wa chakula unaashiriwa na bei ya vyakula sokoni.

Takwimu mbalimbali za Kilimo zimeoneshwa kwenye majedwali yafuatayo:-

Jedwali Na. 1: Eneo la Kilimo

Eneo la Wilaya (Ha)	Eneo la Wilaya Lenye Maji (Ha)	Eneo Linalofaa kwa Kilimo (Ha)	Eneo Linalolimwa (Ha)	Asilimia (%) Eneo Linalolimwa
6,300	0	709	650	91.2

Jedwali Na. 2: Idadi ya familia zinazoshiriki Kilimo

IDADI YA KAYA ZINAZOSHIRIKI KILIMO	IDADI YA WAKULIMA
6,600	27,927 (sensa ya kilimo 2002)

Jedwali Na. 3: Matumizi ya zana za Kilimo

Idadi ya Matrekta madogo	Idadi Ya Matrekta	Asilimia Ya Wakulima Wadogo Wanaotumia Matrekta (%)	Idadi Ya Plau	Asilimia Ya Wakulima Wanaotumia Plau (%)	Idadi Wakulima Wanaotumia La Mkono	Asilimia (%)
6	3	0.5	4	4.5	26,531	95

Changamoto

1. Bajeti finyu ya matumizi mengineyo inayotengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za kilimo, kiasi cha shilingi **10,415,000.00** (milioni kumi na mianne na kumi na tano elfu tukwa mwaka)
2. Baadhi ya vikundi vya wakulima kutokuwa waaminifu kutunza na kutumia fedha za Serikali kulingana na mipango yao. Mfano kikundi cha wakulima Morembe kilichotumia takribani shilingi **4,580,010.00** kwa shughuli zisizokuwa za mradi.
3. Kuendelea kuwepo kwa magonjwa ya mihogo ya batobato na michirizi kahawia kunachangia kupunguza uzalishaji.
4. Kutokunyesha kwa mvua za kutosha katika msimu wa vuli kumechangia kuwepo kwa mavuno hafifu.
5. Wakulima kutozingatia ushauri wanaopewa na wataalamu.

6. Ukosefu wa stadi za kuendesha shughuli za ushirika kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu kwa baadhi ya viongozi wa vyama vya ushirika na kusababisha vyama kutofikia malengo yake
7. Ucheleweshaji wa makato toka kwa waajiri kwa vyama vile vilivyoko katika maeneo ya kazi na kusababisha vyama vilivyokopa fedha benki kushindwa kurejesha mikopo kwa wakati, kukosa mtaji wa kukopeshana na kukosa fedha za kujiendesha.
8. Ucheleweshaji wa makato toka kwa waajiri kwa vyama vile vilivyoko katika maeneo ya kazi na kusababisha vyama vilivyokopa fedha benki kushindwa kurejesha mikopo kwa wakati, kukosa mtaji wa kukopeshana na kukosa fedha za kujiendesha.

Mikakati ya kukabiliana na changamoto

1. Kuwaamuru wanakikundi wa Morembe kurudisha fedha kwenye akaunti ama sivyo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao (maamdalizi ya hatua za kisheria yamekamilika)
2. Wakulima wanashauriwa kutumia mbegu kinzani dhidi ya ugonjwa wa batobato na michirizi ya kahawia, katika msimu wa vuli Halmashauri imenunua **pingili 20,000** za vipando vya mihogo kutokana na mapato yake na kuzigawa kwa wakulima. Halmashauri pia imewahamasisha wakulima kuchangia gharama za ununuzi wa mbegu ya mihogo kinzani kwa ugonjwa wa batobato na Michirizi kahawia kutoka katika gereza la Kiabakali. Wakulima wamechangia jumla ya shilingi **210,000 zilizotosha kununua jumla ya vijiti 10,500.**
3. Wakulima wanahamasishwa kulima mazao yanayostahimili ukame kama vile viazi vitamu na mtama na pia kulima kwa kuweka makinga maji
4. Kuendelea kutoa elimu kwa wakulima kuhusu kanuni bora za kilimo
5. Kuendelea kutoa elimu kwa viongozi na wanachama kupitia mikutano yao mikuu na vikao vya Bodi na kushawishi vyama kuandaa mafunzo mbalimbali kutokana na mapato yao
6. Kuendelea kuwahimiza viongozi kuwachukulia hatua za kisheria wanachama wasio waaminifu katika kurejesha mikopo, ambapo hatua za wali za kisheria zinaendelea kuchukuliwa
7. SACCOS husika kuendelea kuwasiliana na Ofisi ya Mkurugenzi ili aweze kukamilisha malipo ya madeni

6.2. MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma inahudumia wafugaji ambao hufanya ufugaji wa ndani na huduma hizo ni pamoja na:-

- Utambuzi wa magonjwa, ufuatiliaji, utoaji tiba na kinga kama vile chanjo ya kideri cha kuku na chanjo ya kichaa cha mbwa, jumla ya kuku 28,574

walipatiwa chanjo ya Newcastle na kideri, kuku 3,732 chanjo ya fowl pox na mbwa 120 chanjo ya kichaa cha mbwa katika Kata za Manispaa ya Musoma.

- Utoaji ushauri/elimu juu ya ufugaji bora, jumla ya wafugaji 212 wa kuku, ng'ombe, mbuzi na kondoo walipatiwa ushauri wa namna ya kuzingatia kanuni za ufugaji bora katika Kata ya Bweri, Mwisenge, Makoko na Nyakato na maeneo mengine ndani ya Manispaa yetu.
- Ukaguzi wa afya ya mifugo na mazao yake.
Jumla ya mifugo 11,889 (ng'ombe, mbuzi na kondoo) waliruhusiwa kuchinjwa na ukaguzi wa nyama kwa matumizi ya binadamu ulifanyika katika machinjio za Manispaa kwa mwaka 2013/2014, pia kwa mwaka 2014/2015 hadi Januari 2015 jumla ya mifugo 6,455 (ng'ombe, mbuzi na kondoo) waliruhusiwa kuchinjwa na ukaguzi wa nyama kwa matumizi ya binadamu ulifanyika.
- Uboreshaji wa zao la ngozi, Jumla ya vipande vya ngozi 6,930 vilikusanywa kutoka kwa mawakala na kupangwa katika madaraja kabla ya kusafirishwa.

Sambamba na hili Halmashauri katika kuimarisha uboreshaji wa zao la ngozi inajenga banda moja la kukaushia ngozi kwa njia ya chumvi katika eneo la Machinjio ya Bweri.

Wilaya katika kuhakikisha kuwa inakuwa na mifugo yenye afya bora na inayozalisha kwa tija imejiwekea mikakati ifuatayo:-

- Kuongeza idadi ya wataalamu/watumishi wa ugani
- Kuboresha afya ya mifugo kupitia chanjo ili kuzuia magonjwa ya kuambukiza kwa mifugo
- Kuongeza uzalishaji wa samaki kwa njia ya mabwawa.

Takwimu mbalimbali za sekta ya mifugo na uvuvi zimeonyeshwa kwenye majedwali yafuatayo:-

Jedwali Na. 1: Idadi ya Mifugo

Idadi ya Mifugo								
Ng'ombe wa asili	Ngo'mbe wa kisasa	Mbuzi wa asili	Mbuzi wa kisasa	Kondoo	Kuku wa asili	Kuku wa kisasa	Nguruwe	Mbwa na paka
4,870	378	1692	32	173	52000	44650	792	7212

Jedwali Na. 2: Uvuvi wa Samaki

Mwaka	Samaki waliovuliwa	
	Kiasi (kg)	Thamani
2008/2009	23,573,240	30,526,444,000
2009/2010	8,597,136	16,560,976,960
2010/2011	7,321,012	21,431,913,000
2011/2012	6,789,172	16,480,367,340
2012/2013	1,963,647	8,193,439,420
2013/2014	2,311,301	8,942,467,440
2014/2015	2,701,448	9,169,947,470

Takwimu hizi zinaonyesha kuwa kiwango cha samaki kinaendelea kupungua kwa sababu ya uvuvi usiokuwa endelevu. Katika kuhakikisha kuna uvuvi

endelevu wa samaki katika Ziwa Victoria, Wilaya ya Musoma imekuwa inashirikiana na kitengo cha doria Mkoa pamoja na Polisi katika kufanya doria ambazo zimefanikisha kukamatwa makokoro mawili (2) na nyavu kumi (20) ambazo zilikuwa zimeunganishwa mara mbili ambazo kisheria haziruhusiwi.

Jedwali Na. 3: Idadi ya Maafisa Ugani waliopo

(a) Maafisa ugani wa Mifugo

	Waliopo	Mahitaji
Makao Makuu	3	12
Kata	7	16
Mitaa	0	0
Jumla	10	29

Jedwali Na.4: Idadi ya Mashamba darasa

(a) Mifugo

Makao Makuu	0
Kata	3
Mitaa	10
Jumla	10

Mh. Mkuu wa Mkoa,

Katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya (DADPS) katika mwaka wa fedha 2014/2015 Halmashauri kupitia Idara ya Mifugo imetekeleza mpango wa mnyaroro wa thamani kwa kiviwezesha vikundi 3 katika Kata ya Nyamatara na Buhare jumla ya shilingi milioni 15, kila kikundi kimoja shilingi milioni 5 kwa lengo la kuwasaidia kuboresha kuku wao wa asili na kuboresha kipato na lishe. Hadi sasa wako katika hatua tofauti za utekelezaji.

Sambamba na hili, pia Halmashauri kupitia mradi wa LVEMP II inatekeleza miradi miwili katika Halmashauri yetu katika mwalo wa makoko, Kata ya Makoko– kuna mradi wa choo cha kisasa na mradi wa chanja za kuchakata daga katika mwalo wa Nyarusurya, Kata ya Bweri wanaoendelea na mradi wa kuchakata daga.

CHANGAMOTO

Katika utekelezaji wa shughuli za kila siku za miradi ya maendeleo, Idara ya Mifugo na Uvuvi imekuwa inakabiliana na changamoto zifuatazo:-

- i. Upungufu wa fedha za kununulia vifaa/zana za kutekeleza majukumu mbalimbali ya kiofisi na ya nje ya ofisi.
- ii. Kuchelewa kwa fedha za miradi ya maendeleo na hata kutokuletwa kabisa
- iii. Upungufu wa watumishi wa Mifugo na Uvuvi
- iv. Hatuna joshu lolote katika Halmashauri yetu

SULUHISHO / MAPENDEKEZO

- i. Halmashauri kununua boti na injini kwa ajili ya kukusanyia maduhuli ya Halmashauri (leseni za mitumbwi na leseni ya kukusanyia samaki) na kufanya doria kwa ajili ya kudhibiti uvuvi haramu
- ii. Halmashauri kuendelea kuomba kibali cha kuajiri wataalam kwa ajili ya Idara husika.
- iii. Halmashauri kuandaa taratibu za kuwa na joshu

6.3. SEKTA YA USHIRIKA

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ina **vyama vya ushirika 43** vilivyoandikishwa kwa mujibu wa sheria na vina jumla ya **wanachama 10,809**. Hata hivyo ni **vyama 16** tu ndivyo vinafanya shughuli ipasavyo, **vyama 6** vinasuasua na vingine **21** vimeshindwa kabisa kujiendesha licha ya juhudi nyingi zilizofanyika kuvifufua. Pendekezo la kuvifuta limeshawaliishwa kwa Msajiri Msaidizi wa Vyama vya Ushirika. Tumefanikiwa kuandikisha chama cha Ushirika cha Usafirishaji wa Bodaboda. Lengo ni kukuza ajira kwa vijana wa Manispaa ya Musoma.

Mhe. Mkuu wa Mkoa

Vyama hivyo vina mitaji ya **Tsh 22,201,137,619**. Mikopo iliyo kwisha tolewa katika SACCOS ni **Tshs 10,347,875,900** na kiasi cha marejesho ya mikopo hiyo **Tsh. 7,626,543,907**

Mchanganuo wa vyama vya Ushirika na hali ya vyama hivyo katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ni kama ilivyo katika jedwali hapa chini:

Jedwali Na. 1: Idadi ya Vyama vya Ushirika

Aina ya Chama	Idadi ya vyama	Vinavyofanya kazi	Vinavyosuasua	Visivyofanya kazi kabisa
SACCOS	37	15	5	17
Usafirishaji	1	1	0	0
Huduma	4	0	1	3
Viwanda	1	0	0	1
Jumla	43	16	6	21

Jedwali Na. 2 (i): Hali ya vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOS) .

Idadi		Mitaji				Mikopo		
Idadi ya SAC COS	Idadi ya wanachama	Hisa	Akiba	Amana	Jumla	Iliyotolewa	Rejeshwa	Baki
37	10,640	515,500,000	1,537,801,152	126,054,667	2,179,355,819	10,347,875,900	7,626,543,907	2,721,331,993

Jedwali Na.2(ii) Hali ya vyama vya ushirika wa aina nyingine

Idadi		Mitaji
Idadi ya vyama vya aina nyingine	Idadi ya wanachama	Hisa
6	168	21,781,800

CHANGAMOTO:

- i. Kukosa uaminifu kwa baadhi ya wanachama katika kurejesha mikopo
- ii. Ukosefu wa elimu ya ushirika katika kubaini majukumu na uendeshaji wa vyama vya ushirika.

SULUHISHO:

- (i).Kuendelea kuwashauri viongozi kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanaokiuka taratibu
- (ii).Kuendelea kutoa elimu kupitia vikao na mikutano
- (iii).Kuhimiza viongozi kuandaa semina mbalimbali

6.4. BARABARA:

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Wilaya ya Musoma ina jumla ya kilomita 416.58 za mtandao wa barabara kwa mgawanyo ufuatao:-

- Barabara za Lami Kilomita 7.60
- Barabara za Changarawe Kilomita 312.17
- Barabara za Udongo Kilomita 96.81

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ni miongoni mwa Halmashauri za Manispaa na Miji kumi na nane (18) nchini ambazo ziliteuliwa na Serikali kwa ajili ya kuboresha miundombinu mjini kwa kutumia fedha za mkopo wa Benki ya Dunia. Katika Programu hii ambayo imepangwa kwa miaka mitano (5)

kuanzia mwaka **2013/2014** hadi mwaka **2017/2018**, Halmashauri ya Manispaa ya Musoma imetengewa jumla ya Dola za Kimarekani **9,585,615.68** sawa na Tshs. **15,336,985,088.00**.

Katika mwaka **2013/2014** Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ilitengewa na kupokea jumla ya Tshs. **706,730,676.00** ambapo shughuli zifuatazo zimefanyika na zingine zinaendelea kufanyika:-

- Kusanifu kwa kiwango cha lami barabara ya Nyasho – Majita yenye urefu wa kilomita 2.38. kazi hii imekamilika
- Kuandaa Mpango Kabambe wa matumizi bora ya ardhi ambapo Mtalaam mshauri amekamilisha hatua zote nane (8) na kuwasilisha kwenye timu ya wataalamu wa Halmashauri. Kilichobakia ni ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa kuwasilisha mpango ofisi ya mkuu wa mkoa na mkoa kuwasilisha Wizara ya Ardhi, nyumba na maendeleo ya makazi kwa kuidhinishwa kabla ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
- Kujenga uwezo kwa watumishi na wananchi waishio maeneo ambapo miradi itakapotekelzwa. Shughuli hii imefanyika na kukamika.
- Kukarabati ofisi itakayotumika kutunza kumbukumbu za Halmashauri. Shughuli hii imekamilika na ofisi inatumika.
- Kusanifu kwa kiwango cha lami barabara zenye urefu wa kilomita **10.15 (Mutex – Buhare, Kennedy, Karume, Amri Abeid, Makongoro, Maktaba, Serengeti, Uhuru, Lumumba, Kusaga, Rutigingi, Gandhi na Nyasho sokoni – nyasho Majita)**
- Kusanifu soko la Nyasho kazi hii inaendelea.

Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Halmashauri ya Manispaa ya Musoma imetengewa jumla ya Shs 2,606,435,200.00 kutoka Benki ya Dunia ambapo shughuli zifuatazo zimepangwa kufanyika.

- Ujenzi wa barabara ya Nyasho – Majita Mikataba ya Mkandarasi na Mhandisi msimamizi imesainiwa na kazi itanza mwanzoni mwa mwezi Julai, 2015.
- Kujenga uwezo kwa watumishi na waheshimiwa Madiwani ambapo shughuli zinaendelea kutekelezwa.

Aidha Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kila mwaka hupokea fedha kutoka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya matengenezo ya Barabara zilizo chini ya uangalizi wa Halmashauri. Kwa mwaka wa fedha **2013/2014** Halmashauri ya Manispaa iliidhinishwa jumla ya Tshs. **496,060,000.00** toka Mfuko wa Barabara na kupokea jumla ya Tshs. **384,587,844.70** ambazo zilitumika kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- Kulima na kumwaga changarawe sehemu korofi barabara zenye urefu wa kilomita **20 (Mwisenge Makaburini, Bweri, Buhare, Kamunyonge, Kigera, Makoko na Nyamiongo.)**

- Kuziba mashimo kwenye barabara za Lami yenye eneo la mita za mraba **600 (Mukendo, Mwigobero na Kusaga)**
- Kujenga mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa mita **970 (Kigera, Mwisenge Makaburini, Iringo, Kitaji Bweri, Buhare kati)**
- Kujenga kalvati tisa **(9)**.

Kwa mwaka wa fedha **2014/2015** Halmashauri imeidhinishiwa Shs. **1,065,980.00** kutoka mfuko wa barabara kwa ajili ya matengenezo ya barabara. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi **Mei, 2015** Halmashauri ilikuwa imepokea jumla ya Shs. **414,210,692.93** sawa na asilimia 38.9 ya fedha iliyoidhinishwa kwa mwaka mzima.

Aidha utekelezaji wa matengenezo ya Barabara umefanyika kama ifuatavyo;

- (i). Miradi mitatu yenye thamani ya shs.398,884,800/= utekelezaji wake umefikia asilimia 41.3
- (ii). Miradi mitatu yenye thamani ya shs.344,042,500/= Makandarasi wameonyeshwa maeneo ya kazi.
- (iii). Miradi miwili yenye thamani ya shs.202,208,000/= imegawiwa kwa Makandarasi na Bodi ya Zabuni kasha kupitishwa kwenye kamati ya fedha na uongozi kama sheria ya manunuzi inavyoelekeza.

Changamoto

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma upande wa ujenzi inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- Upungufu wa fedha za matengenezo ya barabara hivyo kusababisha barabara zinazofanyiwa matengenezo kutofikia ukamilifu unaotakiwa.
- Fedha kutotolewa kwa wakati na michango michache toka kwa wadau mbalimbali.

6.5. MALIASILI:

6.5.1. Sekta ya Mimiti

Wilaya katika kuhakikisha jamii, taasisi za serikali na vikundi vya mazingira vinashiriki kuotesha na kupanda miche ya miti **500,000** kwa mwaka ina kitalu kinachoendeshwa na Halmashauri ya Manispaa ya Musoma na bustani (8) za vikundi vya kuotesha miche ya miti ya matunda, mbao, vivuli na mapambo. Vikundi vya uoteshaji miche ya miti hujipatia kipato kwa kuuza mche mmoja kati shilingi 100 hadi shilingi 15,000 kutegemeana na aina ya mche.

Wananchi wamekuwa wakiitikia wito wa kupanda miti kila mwaka. Takwimu za upandaji wa miti zinajionesha katika jedwali lifuatalo hapa chini:

Mwaka	2010/2011	2011/2012	2012/2013	2013/2014	2014/2015
Idadi ya Miti	286,406	150,228	236,321	123,586	225,053

Mikakati ya kuhifadhi mazingira ambayo wilaya imejiwekea ni kama ifuatavyo:-

- Kuongeza doria za kusaka wahalifu wa mazingira.
- Kutoa Elimu ya ugani kwa wananchi juu ya uhifadhi wa mazingira
- Kuhamasisha upandaji wa miti ya matunda hasa maparachichi, miembe, machungwa kwenye taasisi hasa shule za Msingi na Sekondari.

6.5.2. Sekta ya Nyuki

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Wilaya inajihusisha na ufugaji wa nyuki kama mbinu ya kupambana na umasikini na ni mojawapo ya huduma za ugani ambazo zimekuwa zikitolewa katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma. Kuna jumla ya vikundi 2 sambamba na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) wanaojishughulisha na ufugaji wa nyuki. Kuna jumla ya mizinga 230 ambayo urinaji wa asali na nta bado haujafanyika.

6.6. MAENDELEO YA ARDHI:

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Sekta ya Mipango Miji na Ardhi

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ina eneo la ukubwa wa kilomita za Mraba 63 kati ya ukubwa huo inakadiriwa kuwa asilimia 80% ya eneo lote limepimwa na asilimia 20% haijapimwa. Asilimia 15% ya eneo lilopimwa linamilikiwa na Jeshi na kiwanja cha ndege.

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kama zilivyo Halmashauri zingine inakabiliwa na tatizo la ujenzi holela (squatter) katika Kata za Nyakato, sehemu ya Kata ya Kigera na Buhare.

Viwanja mbalimbali vimeweza kupimwa na kuidhinishwa kwa matumizi mbalimbali.

Utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

Mwaka upimaji	wa	Viwanja buniwa	Viwanja pimwa	Viwanja kamilishwa
2010/11		2,400	450	450
2011/12		1,500	250	250
2012/13		1,500	500	500
2013/14		600	582	408
2014/15		1,000	449	216

Chanagamoto;

1. Uwepo wa migogoro mikubwa ya ardhi katika Halmashauri yetu ni:-

- Migogoro ya uvamizi wa maeneo ya Serikali mfano kuna uvamizi mkubwa kwenye eneo la shule ya Sekondari Morembe na Musoma Ufundi
 - Migogoro itokanayo na kutoa kiwanja kimoja kwa zaidi ya mtu mmoja ambayo ni ya muda mrefu kuanzia miaka ya 80
 - Gharama kubwa za fidia ya ardhi ambayo husababisha viwanja kuwa ghali kuliko uwezo wa wananchi
2. Udogo wa eneo la Manispaa unaosababisha kukosa maeneo ya huduma mbalimbali muhimu kwa manispaa ya Musoma Mjini kama DAMPO, maeneo ya Viwanda, Mahoteli ya kitalii na Makazi kwa ujumla.

Mikakati ya kuboresha Sekta ya Ardhi

- Kuingia ubia na makampuni yanayopima viwanja ili kupima viwanja vingi ambavyo vitakuwa na bei nafuu
- Kuhakikisha kuwa hakuna “double allocation” tena kwa sasa hivi mtumishi atakayesababisha “double allocation” hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.
- Kushirikiana na Serikali Kuu kupitia mpango wa kurasimisha ardhi “Mkurabita” kuyafanyia “squatter upgrading” maeneo yote yaliyojengwa kiholela.
- Kushirikiana na Mkoa ili Manispaa iweze kuongezewa eneo la utawala toka km za mraba 63 hadi kufikia 665.
- Elimu ya Ardhi pia iendelee kutolewa kwa wananchi kwa wananchi kwa lengo la kupunguza migogoro na uvamizi unaofanywa na wananchi hao.

7.0. HUDUMA ZA JAMII:

7.1. ELIMU YA MSINGI:

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa;

Hali ya utoaji wa Elimu katika wilaya yetu ni nzuri ambapo Wilaya imejitahidi kwa kushirikiana na wananchi kujenga shule za msingi. Wilaya inazo Shule za Msingi kama ifuatavyo:-

Jedwali Na. 1: Idadi ya Shule za Msingi na walimu hadi Sept. 2014:

Idadi ya Shule zote za Msingi (Hadi Sept. 2014)			Idadi ya Walimu wa Shule za Serikali		
SERI KALI	BINAFSI	JUMLA	MAHITAJI	WALIOPO	PUNGUFU
38	8	46	804	741	63

Uandikishaji wanafunzi darasa la kwanza hadi tarehe 31 Machi 2015 kwa watoto wa umri wa miaka saba (7) ulikuwa kama ifuatavyo:-

Tarajiwa			Andikishwa			%
Wavulana	Wasichana	Jumla	Wavulana	Wasichana	Jumla	
2,385	2,779	5,114	2,681	2,798	5,479	107.1

Miundombinu katika elimu ya msingi bado haitoshi kama ambavyo jedwali linavyojionyesha:-

Na.	Aina	Mahitaji	Yaliyopo	Pungufu
1	Vyumba Madarasa	715	398	317
2	Nyumba Walimu	804	42	762
3	Matundu vyoo	1,453	564	889
4	Madawati	12,778	9,972	2,806

Katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi katika mwaka wa fedha **2014/2015** wilaya imetenga Tshs. **294,000,000.00** ikiwa ni kwa ajili ya kutengeneza madawati, kujenga matundu ya vyoo na kujenga vyumba vya madarasa.

Jedwali Na. 2: Mwendoto wa kupangiwa walimu wa Msingi Halmashauri ya Manispaa ya Musoma na walioripoti 2012/13- 2014/2015

WALIOPANGWA	WALIORIPOTI	%
168	167	99.5

Jedwali Na. 3: Matokeo ya Mtihani wa DRS. VII (2014) na waliochaguliwa kuingia Sekondari 2015

Idadi Ya Watahiniwa Drs. Vii (2014)	Waliofaulu	Pass Rate	Waliochaguliwa Sekondari	%	Waliobaki	%
3,620	2,136	59	2,136	100	0	0

Sababu za kupanda kiwango cha ufaulu mtihani drs VII, kutoka 56% (2013) hadi 59%(2014)

- (i) Uwepo wa mitihani ya kujipima ya kutosha
- (ii) Usimamizi na ufuatiliaji wa kazi kwa wanafunzi na walimu kwa ujumla
- (iii) Mafunzo rekebishi kwa wanafunzi wazito.

Mimba mashuleni

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Kutokana na jitihada za Wilaya za kuhakikisha watoto wote wanapata haki yao ya msingi katika sekta ya elimu ya msingi Halmashauri ya Manispaa ya Musoma haina tatizo la mimba kwa wanafunzi shuleni.

MAFANIKIO

Idara ya elimu msingi katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma imepata mafanikio kadhaa yakiwemo haya yafuatayo:-

- (i) Idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa katika shule za msingi wakiwemo wenye ulemavu kuongezeka mwaka hadi mwaka kutoka wanafunzi 306 mwaka 2012 hadi wanafunzi 440 mwaka 2015
- (ii) Uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi kupungua kutoka 1:59 mwaka 2011 hadi 1:46 mwaka 2015
- (iii) Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa taaluma shuleni kwa kuhusisha ngazi za Kata na Wilaya
- (iv) Ukarabati mkubwa unaofanyika katika shule ya msingi Mwisenge ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia yawiane na hadhi ya kuwa ndio shule aliyosomea Baba wa Taifa hayati Mwalimu J. K. Nyerere.
- (v) Ujenzi wa vyumba vya madarasa na ofisi ya walimu katika shule ya msingi Bukanga JWTZ. Kadhalika ujenzi wa vyoo katika shule za msingi Nyarigamba “B”, Buhare, Nyarigamba na Nyakato “B”

Changamoto

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana pia zipo changamoto mbalimbali zinazoikabili idara kama ifuatavyo:-

- (i) Upungufu wa fedha za uendeshaji katika shule za msingi na idarani
- (ii) Upungufu wa samani na miundombinu mbalimbali katika shule zenu
- (iii) Ufinyu wa bajeti inayopokelewa tofauti na inayopitishwa
- (iv) Upungufu wa walimu wataalamu wa fani zote za wanafunzi wenye ulemavu na walimu wa ufundi, vifaa vya kisasa kwa wenye ulemavu na vitabu vyenye maandishi makubwa (large print)
- (v) Ukoekanaji wa chakula shuleni na kushuka kwa kiwango cha taaluma hususani kwa wanafunzi wanaohitaji elimu ya msingi
- (vi) Utunzaji duni wa vifaa na samani za shule
- (vii) Wilaya inakabiliwa na tatizo la uwepo wa jumla ya wanafunzi **1,179** wasiojua stadi za kusoma, kuhesabu na kuandika (KKK) kati ya wanafunzi **32,174** kunakosababishwa hasa na msongamano wa wanafunzi katika vyumba vya madarasa kiasi cha kufanya mwalimu ashindwe kumfatilia mwanafunzi mmoja mmoja na kumsaidia kwa ukaribu ili kumwezesha kumudu stadi hizo kwa kipindi cha somo na muda uliopangwa.

Mikakati ya kutatua changamoto zilizopo

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

- (i) Ufuatiliaji wa mara kwa mara kwa kutembelea shule na kukutana na walimu, wazazi, viongozi wa Serikali za Kata na Mitaa na wadau mbalimbali wa Elimu kwa kuhamasisha uchangiaji wa chakula shuleni ili kuwawezesha wanafunzi kusoma shuleni kwa muda wa kutosha na hivyo kuinua kiwango cha ufaulu kwa shule za msingi za Manispaa.
- (ii) Kuishirikisha jamii katika uchangiaji wa utengenezaji wa madawati kwa kutumia michango, vifaa; ufundi; nguvu kazi; kuendesha harambe na

kuomba misaada kutoka kwa wahisani. Pia kutumia fedha za Halmashauri kiasi cha Tshs. 75,000,000.00 kutengeneza madawati.

- (iii) Kununua vifaa vya kisasa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu (walemavu)
- (iv) Kuendelea kusomesha walimu katika fani mbalimbali za kusaidia wanafunzi wenye mahitaji maalum.
- (v) Tangu mwaka jana shule zote zenye tatizo la uwepo wa wanafunzi wasiojua stadi za kusoma, kuhesabu na kuandika (KKK) zilianzisha madarasa rekebishi (remedial classes) ambayo husaidia kuwafundisha wanafunzi hao kuwawezesha kuelewa stadi hizo kwa wakati ili waende sambamba na wanafunzi wenzao katika darasa. Aidha, wanafunzi hao hupewa vitabu vya ziada ili kujizoeza usomaji wanapokuwa nyumbani.

ELIMU YA SEKONDARI:

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ina jumla ya shule za Sekondari **25** zenye jumla ya wanafunzi **11,915** kati ya hao **7,059** ni wavulana na **4,856** ni wasichana. Shule **18** zinamilikiwa na Serikali na shule **7** siyo za Serikali. Miongoni mwa shule za Sekondari za Serikali Shule **3** zina kidato cha **V** na **VI** na ni za bwani na shule **15** zina kidato cha **I** hadi kidato cha **IV** na ni za kutwa.

7.2.1. IDADI YA SHULE

Idadi ya shule za Sekondari katika Wilaya ya Musoma ni kama ilivyo katika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 1: Idadi ya Shule za Sekondari

KIWANGO	SERIKALI	WATU BINAFSI	JUMLA
KIDATO I – IV TU	15	05	21
KIDATO CHA V – VI	03	02	05
JUMLA	18	07	25

7.2.2. IDADI YA WANAFUNZI WA SEKONDARI

Idadi ya wanafunzi katika shule za Sekondari za Serikali na zisizo za Serikali hadi kufikia mwezi Mei, 2015 ilikuwa kama ilivyo katika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 2: Idadi ya wanafunzi Shule za Sekondari

AINA YA SHULE	WAV	WAS	JUMLA
Shule za Kutwa za Serikali	4,396	3,706	8,102
Shule za Bwani za Serikali	1,514	451	1,965
Jumla ndogo	5,910	4,157	10,067
Shule Binafsi	1,154	694	1,879
JUMLA KUU	7,064	4,851	11,946

7.2.3. IDADI YA WALIMU KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI

Idadi ya walimu katika shule za Sekondari za Serikali imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka ambapo kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Wilaya ya Musoma ilipangiwa jumla ya walimu **08**, kati hao walimu **04** waliripoti na kupangiwa vituo vya kazi. Idadi ya walimu kwa sasa ni kama ilivyo katika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 3: Idadi ya walimu katika shule za sekondari za serikali

Mahitaji	Waliopo	Upungufu
619	485	134

Upungufu wa walimu uliopo ni wa walimu wa masomo ya **Sayansi na Hisabati na** kwa upande wa masomo ya sanaa hakuna upungufu.

7.3.4 MIUNDOMBINU YA SHULE:

Idadi ya miundombinu ya Shule za Sekondari za Serikali ni kama ilivyo katika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 4: Majengo katika Shule za Sekondari

MADARASA			MAABARA			MATUNDU YA VYOO			NYUMBA ZA WALIMU			MAKTABA		
Mahitaji	Yaliyo	Upungufu	Mahitaji	Zilizopo	Upungufu	Mahitaji	Yaliyo	Upungufu	Mahitaji	Zilizopo	Upungufu	Mahitaji	Zilizopo	Upungufu
272	240	32	54	8	46	516	243	273	532	71	461	18	2	16

Jedwali Na. 5: Samani katika Shule za Sekondari

VITI			%	MEZA			%	KABATI			RAFU			%
Mahitaji	Vilivyopo	Upungufu		Mahitaji	Zilizopo	Upungufu		Mahitaji	Zilizopo	Upungufu	Mahitaji	Zilizopo	Upungufu	
10868	10457	411	3.8	10868	10635	233	2.1	200	63	137	237	42	195	

7.3.5 USAJILI WA WANAFUNZI WA KIDATO CHA KWANZA 2015

Wanafunzi waliofaulu mtihani wa darasa la VII mwaka 2014 wanaendelea kuripoti ili kujiunga na kidato cha I. Hadi kufikia tarehe 05 Februari, 2015 Jumla ya wanafunzi **1,539** kati ya **2,243** sawa na **69%** wameripoti shuleni.

Jedwali Na. 6: Usajili wa wanafunzi kidato cha I - 2015

Na	JINA LA SHULE	WALIOPANGWA			WALIORIPOTI			%	WASIORIPOTI			%
		ME	KE	JML	ME	KE	JML		ME	KE	JML	
1	Nyasho	52	41	93	34	27	61	66	18	14	32	34
2	Nyamiongo	49	55	104	39	24	63	61	10	31	41	39
3	Mukendo	65	57	122	33	24	57	47	32	33	65	53
4	Bweri	84	79	163	74	75	149	91	10	4	14	9
5	Nyabisare	77	35	112	41	17	58	52	36	18	54	48
6	Buhare	107	88	195	68	56	124	64	39	32	71	36
7	Mshikamano	72	58	130	68	54	122	94	4	4	8	6
8	Baruti	69	57	126	49	39	88	70	20	18	38	30
9	Kiara	105	113	218	92	82	174	80	13	31	44	20
10	Morembe	59	59	118	49	50	99	84	10	9	19	16
11	Kamunyonge	68	48	116	51	34	85	73	17	14	31	27
12	Musoma ufu.	120	0	120	95	0	95	79	25	0	25	21
13	Makoko	110	105	215	60	54	114	53	50	51	101	47
14	Mwisenge	102	77	179	69	58	127	71	33	19	52	29
15	Nyamitwebiri	82	64	146	47	41	88	60	35	23	58	40
16	Iringo	38	47	85	20	15	35	41	18	32	50	59
	Jumla	1260	983	2243	889	650	1539	69	371	333	704	31

7.3.6 MPANGO WA CHAKULA CHA MCHANA SHULENI

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma inaendelea na mpango wa wanafunzi kupata chakula cha mchana shuleni. Katika kutekeleza mpango huu tunaendelea kuhamasisha wazazi na jamii kwa ujumla ili kuchangia chakula cha mchana kwa wanafunzi katika shule za Sekondari za kutwa.

Hadi sasa shule **2** za Sekondari (**Iringo na Kiara**) zimekwishaanza kutoa chakula cha mchana kwa wanafunzi na walimu na wanafunzi hubaki shuleni hadi saa 11.00 jioni. Tunaendelea kuhamasisha jamii kupitia vikao vya wazazi na Bodi za shule kwa lengo la kuhakikisha kuwa shule zote zinatoa chakula cha mchana kwa wanafunzi. Tunatoa wito kwa wakazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kuunga mkono mpango huu ili kuwezesha kuinua kiwango cha ufaulu.

7.3.7 HALI YA UFAULU WA MITIHANI YA KITAIFA

Ufaulu wa mitihani ya Kitaifa umeongezeka kutoka **40.1%** mwaka **2012** hadi kufikia **58.3%** mwaka **2013**. Mikakati ya kuboresha Elimu inaendelea sambamba na uboreshaji wa hali ya ufundishaji na ujenzi wa miundombinu katika shule za Sekondari. Kwa sasa hakuna mwanafunzi asiyejua kusoma, kuandika na kuhesabu aliyejiunga na Shule ya sekondari. Hali ya ufaulu katika mitihani ya Kitaifa ya kidato cha IV na VI kwa kipindi cha miaka mitano ni kama ilivyo katika majedwali yafuatayo:

Jedwali Na. 7: MATOKEO YA KIDATO CHA IV MWAKA 2005-2013

S/N	MWAKA	WALIOSAJILIWA			WALIOFANYA			WASIOFANYA			MADARAJA					% UFAULU (DIV I - IV)
		ME	KE	JML	ME	KE	JML	ME	KE	JML	I	II	III	IV	O	
1	2005	544	302	846	528	296	824	16	5	21	73	68	138	399	138	82%
2	2006	466	300	766	461	296	757	5	4	9	54	65	130	376	130	82.5%
3	2007	644	284	928	637	267	904	7	17	24	65	102	157	390	136	79%
4	2008	726	296	1022	710	285	995	17	10	27	61	88	158	528	140	84%
5	2009	1200	916	2116	1158	864	2022	42	49	91	34	80	202	941	727	62%
6	2010	1590	1058	2648	1515	1005	2520	45	53	98	60	84	211	765	1430	44%
7	2011	1709	741	2450	1640	724	2364	69	17	86	22	85	172	953	1094	53%
8	2012	1618	986	2604	1592	896	2488	26	90	116	32	69	142	754	1287	40.1%
9	2013	1527	887	2414	1463	847	2310	54	40	94	56	144	292	753	1245	58.3%
	Jumla	10024	5770	15794	9704	5480	15184	281	285	566	457	785	1602	5859	6327	65

Jedwali Na. 8: MATOKEO YA KIDATO CHA VI MWAKA 2005-2013

S/N	MWAKA	WALIOSAJILIWA			WALIOFANYA			WASIOFANYA			UFAULU KIMADARAJA					% UFAULU (DIVI. I - IV)
		ME	KE	JML	ME	KE	JML	ME	KE	JML	I	II	III	IV	O	
1	2005	138	2	140	137	2	139	1	0	1	29	53	46	6	5	96
2	2006	192	8	200	189	8	197	3	0	3	29	66	78	20	3	97
3	2007	321	33	354	320	33	353	1	0	1	44	73	143	77	17	95
4	2008	496	44	540	495	44	539	1	0	1	58	155	231	77	18	96
5	2009	364	81	445	360	80	440	4	1	5	34	107	233	47	19	95
6	2010	442	88	530	442	87	529	0	1	1	32	123	288	58	28	94
7	2011	573	116	689	571	116	687	2	0	2	27	130	392	93	45	93
8	2012	448	112	560	448	112	560	0	0	0	14	118	350	52	26	95
9	2013	467	89	556	467	88	555	0	1	1	8	84	413	39	11	98
	Jumla	3441	573	4014	3429	570	3999	12	3	15	275	909	2174	469	172	95.4

7.3.7 Mimba mashuleni.

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Pamoja na Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kufanya jitihada za kudhibiti mimba shule za sekondari, bado tatizo lipo katika shule za sekondari na hivyo jitihada zinaendelea kufanywa na Halmashauri ili wananchi na wazazi kwa ujumla waweze kutambua umuhimu wa elimu kwa watoto wa kike. Jedwali lifuatalo linaonesha matukio ya mimba katika shule za sekondari kuanzia Mwaka 2012 hadi 2014:-

Jedwali Na. 9: Mimba katika shule za Sekondari

Idadi			Waliofikishwa mahakamani			Waliofikishwa baraza la kata		
2012	2013	2014	2012	2013	2014	2012	2013	2014
4	5	1	0	1	0	2	1	1

7.3.8 MPANGO MKAKATI WA UJENZI WA MAABARA

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Ujenzi wa maabara katika Halmashauri ya Musoma unatekelezwa kwa kuzingatia agizo la Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kila shule kuwa na maabara tatu za sayansi.

Utekelezaji wa agizo hilo ulianza kwa ushirikiano kati ya viongozi wa Wilaya ya Musoma, viongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma na Wadau mbalimbali wa maendeleo katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.

Mnamo tarehe 18 Septemba, 2014 kikao cha Wadau wa Elimu kiliitishwa katika ukumbi wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma. Katika kikao hicho taarifa ya hali ya Elimu katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma iliwasilishwa. Taarifa hiyo ilionyesha hali halisi na mahitaji ya miundombinu ya shule za Sekondari na Msingi. Aidha katika kutafuta utatuzi wa changamoto ya upungufu wa miundombinu ya elimu suala la ujenzi wa maabara katika shule za Sekondari lilipewa kipaumbele.

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Kwa mujibu wa taarifa hiyo jumla ya vyumba vya maabara 46 vilitakiwa kujengwa na gharama ya kila maabara moja pamoja na vifaa vyake ilikadiriwa kuwa shilingi **milioni 75** sawa na shilling **3,450,000,000.00** kwa maabara **46**. Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwenye bajeti ya mwaka 2014/2015 ilipanga kutumia shilingi **409,775,000.00** na kiasi hiki kilipatikana baada ya kubadili matumizi ya vifungu vingine vya miradi ya maendeleo vilivyokuwa vimetengewa fedha kwenye Bajeti yake ya mwaka 2014/2015 ambapo shilingi **47,000,000.00** ilikusudiwa zitokane na mapato ya ndani na shilingi **362,775,000.00** ruzuku kutoka Serikali kuu.

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Hata hivyo baada ya kuona kuwa uwezekano wa kupata kiasi hicho cha fedha kilichokadiriwa kujenga maabara mpya ni mdogo, Halmashauri ya Manispaa ya Musoma iliamua kubadili vyumba vya madarasa kuwa maabara hasa kwenye shule ambazo hazikuwa na upungufu wa vyumba vya madarasa. Jumla ya vyumba vya madarasa **36** vilipitishwa kubadilishwa kuwa maabara na vyumba vya maabara **10** vilitakiwa kukamilishwa.

Ili kubadili chumba cha darasa kuwa maabara ilishauriwa kuwa kila chumba cha darasa kiongezewe chumba kidogo kwa ajili ya maandalizi (preparation room).

Gharama ya kubadili vyumba vya madarasa **36**na kukamilisha maabara **10** ilikadiriwa kuwa shilingi **821,020,600/=**.

Aidha baada ya taarifa ya Elimu kuwasilishwa Wadau wa Elimu waliijadili na kisha kushauri kuwa ni muhimu wadau mbalimbali washirikishwe kuchangia ujenzi wa maabara hizo.

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Mnamo tarehe 23 Septemba, 2014 kikao cha Wadau wa Maendeleo kiliitishwa, katika kikao hicho wadau wote waliona umuhimu wa kujenga maabara na waliahidi kuchangia fedha na vifaa vya ujenzi ambapo kwa siku hiyo zilitolewa ahadi za jumla ya shilingi zipatazo **24,500,000.00** na mifuko ya saruji ipatayo **218**. Pia wajumbe wa kikao hicho waliamua kuunda kamati ya kusimamia mpango mzima wa ujenzi wa maabara; ambapo Mwenyekiti wa kamati hiyo ni Mkuu wa Wilaya na Katibu wake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.wajumbe ni Mh. Mbunge, Mtahiki Mayor, Naibu Mayor na wawakilishi 12 wa wadau wa maendeleo.

Katika kusimamia ujenzi wa maabara kamati inafanya majukumu yafuatayo:-

- i. Kukusanya michango kutoka kwa wadau na kufuatilia ahadi mbalimbali zilizoahidiwa,
- ii. Kusimamia matumizi ya michango ya ujenzi wa maabara na kufuatilia kuhakikisha kuwa fedha zote zinazokusanywa zinafanya kazi iliyokusudiwa.

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Wananchi, mashirika, taasisi, madhehebu ya dini na makampuni mbalimbali wameonyesha moyo wa dhati katika kuchangia ujenzi wa maabara.

Hadi kufikia tarehe 06/02/2015 jumla ya shilingi **160,556,800.00** zimekusanywa, kati ya hizo shilingi **111,650,000/=** ni mchango wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma na Tsh. **48,906,800.00** na mifuko ya saruji **75** zinatokana na michango ya wananchi na wadau mbalimbali.

Hadi kufikia tarehe 05/02/2015 jumla ya shilingi **159,645,000.00** na mifuko **75** ya saruji vimetumika katika ujenzi wa maabara. Fedha hizo na mifuko ya saruji

vilipelekwa kwenye Kata na WDC ndiyo inaosimamia ujenzi wa maabara hizo ngazi ya Kata. Mgawanyo wa fedha na saruji pamoja na hatua ya ujenzi kwa kila shule inafafanuliwa kwenye Jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 10: Matumizi ya fedha za ujenzi wa maabara na hatua za ujenzi

Na	JINA LA SHULE	SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA	UTEKELEZAJI	VIFAA VILIVYOPE LEKWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOTU MIKA (Tsh.)
1	Mukendo	-Kujenga vyumba 3 vya maabara kwa ajili ya matayasisho.	-Vyumba 2 vya maabara kwa ajili ya matayarishovimepigwa bati na chumba 1 kimejengwa hadi usawa wa mtambaa panya	Saruji mifuko 20	12,750,000.00
2	Nyasho	-Kujenga vyumba 2 vya maabara kwa ajili ya matayasisho na kujenga chumba 1 kipya cha maabara.	-Vyumba 2 vya maabara kwa ajili ya matayasisho vimejengwa na vimepigwa bati -Msingi wa maabara mpya 1 umejengwa.	Saruji mifuko22	11,000,000.00
3	Mshikamano	-Kujenga vyumba 2 vya maabara kwa ajili ya matayasisho	-Vyumba 2 vya maabara kwa ajili ya matayarisho vimejengwa, kupauliwa na kupigwa plasta	Saruji mifuko20	11,568,000.00
4	Morembe	-Kujenga vyumba 2 vya maabara kwa ajili ya matayarisho	-Vyumba 2 vya maabara kwa ajili ya matayarisho vimejengwa na kupauliwa.		9,500,000.00
5	Buhare	-Kujenga vyumba 2 vya maabara kwa ajili ya matayarisho	-Vyumba 2 vya maabara kwa ajili ya matayarisho vimejengwa, vimeezekwa na kupigwa lipu		12,065,000.00

6	Nyamiongo	-Kujenga vyumba 2 vya maabara kwa ajili ya matayarisho -Kujenga maabara 1 mpya	- Vyumba 2 vya maabara kwa ajili ya matayarisho vimepigwa bati na kuanza kupigwa lipu -Msingi wa maabara mpya 1 umejengwa	Saruji mifuko 13	12,200,000.00
	Kiara	Kupiga lipu vyumba 3 vya maabara	Vyumba 3 vya Maabara vimepigwa lipu kwa nje na kuchapiwa ndani		5,880,000.00
8	Iringo	- Kujenga vyumba 2 vya maabara kwa ajili ya matayarisho. - Kujenga maabara 1 mpya	- Vyumba 2 vya maabara kwa ajili ya matayarisho vimejengwa hadi usawa wa renta. - Msingi wa maabara 1 umekamilika		9,200,000.00
9	Mwisenge	-Kujenga chumba 1 cha maabara kwa ajili ya matayarisho -Kuweka dari vyumba 2 vya maabara -Kubandua na kuweka sakafu upya kwenye maabara 2	- Chumba 1 cha maabara kwa ajili ya matayarisho kimejengwa hadi usawa wa renta -Uwekaji wa mbao za dari kwenye maabara 2 umekamilika. - Ubanduaji wa sakafu kwenye maabara 2 umekamilika		8,726,000.00
10	Songe	-Kujenga vyumba 2 vya maabara kwa ajili ya matayarisho	-Vyumba 2 vya maabara kwa ajili ya matayarisho vimejengwa na kupigwa bati		8,000,000.00
11	Nyabisare	-Kujenga vyumba 3 vya maabara kwa ajili ya matayarisho	-Vyumba 2 vya maabara kwa ajili ya matayarisho vimepigwa bati na 1 kimejengwa hadi usawa wa renta		12,000,000.00
12	Nyamitwebiri	-Kujenga vyumba 2 vya maabara kwa ajili ya matayarisho	-Vyumba 2 vya maabara kwa ajili ya matayarisho vimejengwa na kupigwa bati.		8,000,000.00
13	Makoko	-Kupiga lipu ndani na nje vyumba 3 vya maabara	-Vyumba 3 vya maabara vimepigwa lipu ndani na nje		8,426,000.00

14	Baruti	-Kujenga vyumba 3 vya maabara kwa ajili ya matayarisho	-Vyumba 3 vya maabara kwa ajili ya matayarisho vimejengwa hadi usawa wa mtambaa panya		11,035,000.00
15	Bweri	-Kujenga chumba 1 cha maabara kwa ajili ya matayarisho -Kupiga lipu chumba 1 cha maabara -Kuandaa na kuweka fremu 5 za madirisha na 3 za milango	-chumba 1 cha maabara kwa ajili ya matayarisho kimejengwa na kupigwa bati -Fremu 5 za madirisha na 3 za milango zimeandaliwa na kuwekwa kwenye maabara		6,700,000.00
16	Kamunyonge	-Kujenga vyumba 2 vya maabara kwa ajili ya matayarisho	-Vyumba 2 vya maabara kwa ajili ya matayarisho vimejengwa hadi usawa wa mtambaa panya		8,000,000.00
17	Mara	Kujenga chumba 1 cha maabara kwa ajili ya matayarisho	-Chumba 1 cha maabara kwa ajili ya matayarisho kimejengwa hadi usawa wa mtambaa panya		3,250,000.00
		Matumizi mengineyo (chakula, usafiri, na posho)			846,000.00
		JUMLA		Mifuko 75	159,645,000.00

7.2.2.1. HALI YA UJENZI WA MAABARA

Hali halisi ya ujenzi wa maabara katika Shule za Sekondari za Serikali kwa sasa ni kama ilivyo katika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 11: Hali ya utekelezaji wa ujenzi wa maabara katika Shule za Sekondari za Halmashauri ya Manispaa ya Musoma hadi tarehe 31/01/2015

Na.	Jina la Shule	Mahitaji	Hali ya Maabara	Hali ya Majengo/Vyumba ambavyo vimekamilika na ambavyo havijakamilika					
			Maabara zenye samani, mifumo ya maji, Gesi na zana muhimu	Chumba kamilika bila Samani	Pauliwa/Ezekwa	Hatua ya Lenta	Hatua ya Msingi/Jamvi	Uchimbaji wa Msingi	%
1	Baruti	3			3				55
2	Buhare	3			3				55
3	Bweri	3		2	1				75
4	Iringo	3			2	1			41
5	Kamunyonge	3	1		2				76
6	Kiara	3			3				55
7	Morembe	3	1		2				76
8	Makoko	3			3				55
9	Mshikamano	3			3				55
10	Musoma Tech	3	3						100
11	Nyamiongo	3			2		1		40
12	Mukendo	3			3				40
13	Songe	3			3				55
14	Mara	3	2		1				76
15	Nyasho	3			2	1			41
16	Nyamitwebiri	3	1		2				76
17	Nyabisare	3			3				55
18	Mwisenge	3			3				55
	Jumla	54	8	2	41	2	1	0	64

Jitihada za kukusanya fedha na vifaa vya ujenzi kutoka kwa wadau mbalimbali zinaendelea.

7.2.4.2. CHANGAMOTO

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Halmashauri inakabiliwa na changamoto zifuatazo katika ujenzi wa maabara:-

- Kiasi cha fedha cha shilingi **1,500/=** kinachoidhinishwa kila mwaka kwa ajili kulipia gharama za chakula, maji na umeme kwa wanafunzi wa bweni hakitoshi. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2014 shule za Sekondari za bweni zilikuwa zinadaiwa na wazabuni jumla ya shilingi **817,290,212.79**, deni hili mpaka sasa bado halijalipwa na Wazabuni wamegoma kutoa huduma tangu mwezi January, 2014.
- Kukosekana kwa gari la idara ya Elimu Sekondari kunaathiri ufuatiliaji wa shughuli za kila siku katika shule za Sekondari.
- Uvamizi wa maeneo ya shule unaofanywa na baadhi ya wananchi.
- Baadhi ya wanasiasa kupinga uchangiaji wa ujenzi wa maabara kwa kauli wanazozitoa wakiwa kwenye mikutano yao ya siasa. Kauli hizi zimesababisha baadhi ya wadau na wananchi waliokuwa na nia ya kuchangia ujenzi wa maabara wasite na wengine kuacha kabisa kutoa michango.
- Fedha zilizotengwa na Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa maabara hazijapatikana zote kutokana na Serikali Kuu kutotoa fedha za maendeleo kwa wakati.
- Wananchi na baadhi ya makampuni yaliyotoa ahadi ya vifaa na fedha kwa ajili ya ujenzi wa maabara hawajakamilisha ahadi zao licha ya kufuatiliwa mara kwa mara.
- Utoro wa rejareja kwa wanafunzi shuleni.

7.2.4.3. MIKAKATI YA KUKAMILISHA UJENZI WA MAABARA

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma imejiwekea mikakati ifuatayo kwa ajili ya kuiwezesha kukamilisha ujenzi wa maabara:-

- Tunaishauri Serikali iongeze bajeti ya chakula kutoka shilingi 1500/= kwa siku hadi walau shilingi 2500/= na pia iwalipe wazabuni madai yao mapema.
- Halmashauri ya Manispaa ya Musoma imepanga kupeleka maombi maalum ya gari wakati wa kuwasilisha bajeti ya mwaka 2015/2016.
- Halmashauri ya manispaa inaendelea na mpango wa kupima na kumilikisha maeneo ya shule za Sekondari kwa kutenga bajeti ya kupima maeneo kila mwaka.
- Kuendelea kuhimiza michango ya ujenzi wa maabara kutoka wadau mbalimbali.
- Kufuatilia fedha za miradi toka Serikali Kuu ili ziweze kutumika kwenye ujenzi wa maabara.
- Kuendelea kutoa Elimu ya umuhimu wa maabara za Sayansi kwa jamii ya wakazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma, na Taifa kwa ujumla.

7.2 HUDUMA ZA AFYA:

VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA

Halmashauri ya Manispaa ina jumla ya vituo 26 vya kutolea huduma za afya katika mchanganuo ufuatao:

Jedwali Na: 1: Vituo vya kutolea huduma za afya (S=Serikali, B=Binafsi, na MD=Mashirika ya Dini)

Hospitali				Vituo vya Afya				Zahanati			
S	MD	B	Jumla	S	MD	B	Jumla	S	MD	B	Jumla
1	0	0	1	2	1	3	5	11	4	6	20

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ina jumla ya maduka ya dawa muhimu 80 na pharmacy 5. Aidha tunategemea kufungua zahanati ya Nyamatare ambayo ujenzi wake upo kwenye hatua za mwisho.

RASILIMALI WATU YA IDARA

Idara ya afya manispaa ya Musoma ina jumla ya watumishi wapatao 178 mpaka kufikia Mei 2015. Watumishi hawa wanajumuisha watumishi wa idara ya afya kinga na tiba.

HALI YA UTENDAJI KAZI

WAGONJWA WALIOHUDUMIWA

Katika kipindi cha mwaka 2014, jumla ya wagonjwa **137,139** kama wagonjwa wa nje waliweza kupatiwa huduma za afya katika vituo vyetu. Kati ya hao wanawake ni **82,234** na wanaume ni **54,905**. Kwa upande wa wagonjwa wa waliolazwa jumla ya wagonjwa **9,522** walilazwa, kati ya hao wanaume ni **3,808** na wanawake ni **5,714**

MAGONJWA 10 YANAYOSUMBUA

Magonjwa kumi yanayosumbua wananchi wa manispaa ya Musoma ni kama ifuatavyo:

Na.	UGONJWA	IDADI	ASILIMIA
1	Malaria	41,239	45
2	magonjwa ya mfumo wa mkojo (UTI)	18,641	20
3	Minyoo	15,938	17
4	Majeraha na ajali	3,568	4
5	Vichomi	3,056	3
6	Kichocho	2,955	3
7	Magonjwa ya via vya uzazi	2,223	2
8	Magonjwa ya moyo	1,880	2
9	Magonjwa ya ngono	1,836	1.9
10	Magonjwa ya njia ya hewa	999	1
	JUMLA	92,335	

HUDUMA ZA UZAZI KWA AKINA MAMA, BABA NA MTOTO (RCH SERVICES)

Manispaa ya Musoma ina jumla ya vituo 17 vinavyotoa huduma za mama, baba na mtoto. Katika kipindi cha mwaka 2014, jumla ya akina mama wajawazito waliohudhuria kliniki walikuwa 15,272 (92%) kati ya akina mama 15,578 waliotarajiwa.

Aidha jumla ya akina mama 1,441 walijifungua salama katika vituo vyetu, na 29 walipewa rufaa kwa ajili ya matibabu zaidi. Viwango vya chanjo zote kwa akina mama na watoto chini ya miaka mitano ni 98%. Huduma ya uzazi wa mpango katika Halmashauri yetu ni 87% kwa njia zote fupi na za muda mrefu.

Kwa kipindi cha mwaka 2014, kumetokea jumla ya vifo 19 vya akina mama wajawazito na vifo 79 vya watoto wachanga chini ya miaka mitano. Vifo vyote hivi vimetokea katika Hospitali ya Mkoa wa Mara.

UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA MKOA WA KUPUNGUZA VIFO VYA AKINA MAMA WAJAWAZITO NA WATOTO WACHANGA

Mhe.Mkuu wa Mkoa, Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ilianza kutekeleza Mkakati wa Mkoa wa kupunguza vifo vya akina mama wajawazito na watoto wachanga tangu Julai 2013. Kwa mujibu wa mkakati huo, lengo la Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ilikuwa ni kupunguza vifo vya akina mama kutoka 20 mwaka 2012 hadi 10 ifikiapo mwaka 2016. Katika lengo kuu hilo kuna malengo mahsusi (**specific objectives**) sita (6) yafuatayo;

1. Kuboresha vituo vya afya ili viweze kutoa huduma ya kujifungua kwa njia ya kupasuliwa na kuongeza damu salama.
2. Kusajili wanawake wote wajawazito na kuwafuatilia ili waende kliniki na kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma.
3. Kuwahimiza akina mama wajawazito baada ya kujifungua wajiunge na uzazi wa mpango.
4. Kuboresha mfumo wa rufaa za wagonjwa.
5. Kuongeza idadi ya watumishi wa kada ya Afya.
6. Kuboresha vikao vya ngazi ya kata na mitaa kwa ajili ya kujadili taarifa za utekelezaji

Mhe.Mkuu wa Mkoa, Tangu Julai 2013, Manispaa ya Musoma imefanya yafuatayo katika kutekeleza malengo mahsusi yaliyotajwa hapo juu:

- I. Vifo vimepungua kutoka 20 mwaka 2012/2013 mpaka 14 kwa kipindi cha Julai, 2014 - Mei, 2015. Vifo hivi vyote hutokea katika Hospitali ya Mkoa, na nusu ya

vifo hivyo si vya wakazi wa Manispaa ya Musoma. Vyanzo vikuu vya vifo hivyo ni kuchelewa kufikishwa Hospitalini na upungufu wa damu.

- II. Vikao viwili vimefanyika kwa maafisa watendaji wa kata 13 na wa mitaa 57 kwa kutoa maelekezo mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa mkakati huu.
- III. Motisha ya Tsh.10, 000/= inatolewa kwa waganga na wauguzi wanaozalisha vituoni ili kuongeza kiwango cha uzalishaji.
- IV. Akina mama waliojifungua wanaendelea kufuatiliwa baada ya saa 24, siku 7, siku 28 na siku 42 ili kujiridhisha na afya ya mama na mtoto wake.
- V. Katika kipindi hicho, Jumla ya watumishi wa afya 34 wa kada mbalimbali wameajiriwa na wote wapo kazini mpaka sasa na mkakati wa kuwatunza upo. Pia watumishi 11 wamepelekwa katika vyuo mbalimbali vya afya ili kuongeza ujuzi wao.
- VI. Mfumo wa rufaa umeboreshwa kwa kuwa na magari ya wagonjwa (ambulance) mawili ambayo yanatoa huduma muda wote (saa24) katika vituo vyote vilivyopo katika manispaa yetu.
- VII. Kituo cha Afya Nyasho kimeboreshwa kwa kukarabati vyoo vya wagonjwa wa nje matundu 6, kununua vitanda vya kuzalishia na vya wagonjwa wa kawaida, kununua vyandarua na mashuka, kuongeza upatikanaji wa dawa ikiwa ni pamoja na kuimarisha stoo ya madawa. Nyumba ya upasuaji pamoja na vifaa vyake viko tayari inasubiri kufunguliwa.

HUDUMA ZA UKIMWI NA KIFUA KIKUU

Pamoja na huhudi zetu katika mapambano dhidi ya UKIMWI, bado hali ya maambukizi ya UKIMWI yako juu ya kiwango cha taifa ambacho ni 5.1% wakati kiwango cha maambukizi katika Halmashauri yetu ni 5.3%. Sababu kubwa za kiwango hiki kikubwa ni pamoja na maeneo ya uvuvi, matumizi ya madawa ya kulevya na ngono zembe. Juhudi mbalimbali zinaendelea kufanyika katika kupambana na maambukizi mapya, zikiwemo, kuendelea kutoa elimu ya jinsi ya kujikinga na maambukizi, kuendelea kutoa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI (ARVs) pamoja na kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT). Kwa upande wa KIFUA KIKUU, kwa mwaka 2014, jumla ya wagonjwa 229 waligundulika kuwa na maambukizi ya kifua kikuu, kati ya hao wagonjwa 79 waliweza kutibiwa na kupona. Hivyo jumla ya wagonjwa 150 bado wanaendelea na matibabu katika kliniki zetu.

HALI YA UGONJWA WA MALARIA

Kama ilivyoielezwa hapo awali, malaria bado ni ugonjwa unaoongoza kwa wingi katika makundi yote ya wagonjwa wale wa nje na waliolazwa. Mpaka sasa kiwango cha malaria katika manispaa ya Musoma ni 42%. Kutokana na hali hii, Manispaa ya Musoma kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa afya imeweka afua afua kadhaa za kupambana na ugonjwa huu; zikiwemo zifuatazo.

1. Kugawa vyandarua vya bure kwa wananchi
2. Kutoa dawa za kupambana na malaria kwa akina mama wote wajawazito wanaohudhuria kliniki.
3. Aidha kuanza Julai 2015, wilaya yetu itatekeleza mradi wa kuuva viuatilifu vya malaria katika maeneo yote yenye mazalia ya mbu.

TAARIFA YA MFUKO WA AFYA YA JAMII (CHF)

Mhe. Mkuu wa Mkoa, Mfuko wa afya ya jamii, katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa sasa uma jumla ya kaya **810 (11.8%)**, hii ni kwa mujibu wa takwimu za hadi mwezi Machi 2015. Zahanati na vituo vya afya ndivyo vinahusika na usajili wa wanakaya, hivyo utendaji wa kila kituo ni kama ifuatavyo:-

SN	JINA LA KITUO	NAMBARI YA AKAUNTI	KAYA TARAJIWA	KAYA ZILIZOJIUNGA	ASILIMIA
1.	MWISENGE DISPENSARY	3031200058	558	179	32
2.	MAKOKO DISPENSARY	3031200076	669	82	12.2
3.	BWERI HEALTH CENTER	3031200057	780	152	19.4
4.	IRINGO DISPENSARY	3031200060	781	107	13.7
5.	BUHARE DISPENSARY	3032301969	478	56	11.7
6.	KWANGWA DISPENSARY	3031200074	646	58	8.9

7.	NYASHO/NYAMATARE HEALTH CENTER	3031200059	1539	131	8.5
8.	NYAKATO DISPENSARY	3031200075	781	38	4.8
9.	RWAMULIMI DISPENSARY	3031603956	604	7	1.1
	JUMLA		6836	810	11.8

HALI YA DAWA VITUONI

Upatikanaji wa dawa katika vituo vyetu ni kurudhisha hasa kwa dawa muhimu (essential medicine) kama dawa za malaria za mseto, chanjo, viua sumu (Antibiotics) kama Amoxylin, dawa za minyoo ya tumbo (Albendazole) dawa za kuongeza maji kwa watoto wanaoharisha (ORS), vipimo vya haraka vya malaria (MRDTs) na dawa za uzazi wa mpango. Hii imetokana na Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kupata dawa kutoka Bohari kuu ya Dawa (MSD) na kununua dawa kwa Fedha za Mfuko wa Pamoja wa Afya (**Health Basket Fund**). Pia, vituo vimekuwa vikinunua dawa zinazokosekana kwa kutumia fedha za Bima ya Afya (NHIF) na makusanyo ya papo kwa papo (user fee).

MATIBABU YA WAZEE

Manispaa ya Musoma inatoa huduma za afya kwa wazee katika vituo vyake vya kutolea huduma bure kulingana na sheria na miongozo ya serikali. Ili kurahisisha matibabu ya kundi hili, idara ya afya iliandaa utaratibu wa kuwatambua na kuwapatia vitambulisho wazee ili waweze kupata urahisi wa huduma za afya. Zoezi la utambuzi liliweza kufanyika mwaka 2013 kwa kushirikiana na idara ya maendeleo ya jamii na chama cha wazee (SAWATA) katika kata za Nyasho, Kamnyonge, Kigera, Iringo na Mwigobero ambapo jumla ya wazee **83** waliweza kutambuliwa na wote **83** wameweza kupatiwa vitambulisho vya matibabu. Awamu ya pili ya utambuzi bado inaendelea katika kata zote za Manispaa.

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI IDARA

1. Ukosefu wa gari la kufanyia shughuli za usimamizi elekezi na kazi nyingine za Idara.
2. Wengi wa wagonjwa wa katika vituo vya kutolea huduma kutokana na ukosefu wa Hospitali ya Manispaa.

3. Upungufu mkubwa wa watumishi wa Afya usiokidhi idadi ya wagonjwa tunaowahudumia.
4. Mwitikio mdogo wa wananchi katika kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF)
5. Kuchelewa kwa mapokezi ya dawa kutoka MSD, hata wanapoleta hazikidhi mahitaji.

MIKAKATI YA KUZIONDOA

1. Kufanya uhamasishaji wa wananchi kujiunga na Mfuko wa Afya Jamii ili kukabiliana na upungufu wa dawa vituoni.
2. Kuendelea kuomba watumishi kupitia bajeti ili kukabiliana na upungufu uliopo.
3. Kuongeza vituo vya kutolea huduma za afya mfano ufunguzi wa Zahanati ya Nyamatara na kukamilisha ujenzi wa Zahanati ya Rwamlimi.

7.3 HUDUMA ZA MAJI:

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Wakazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma wanapata huduma ya maji kwa matumizi ya binadamu inayotolewa na Mamlaka ya Maji Safi Musoma (MUWASA). Wakazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma wanaopata huduma ya maji kutoka mfumo rasmi wa MUWASA ni asilimia 76.

Tunapenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuhakikisha kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma inapata maji ya kutosha na yaliyo salama na safi kwa kuwezesha kutekelezwa kwa mradi mkubwa wa maji unaoendelea kujengwa katika Manispaa yetu ya Musoma. Tunaamini kuwa bila ya juhudi zake mradi huu usingewezekana kujengwa.

Aidha Halmashauri inaendelea na uhamasishaji wa wananchi kutambua umuhimu wa kuvuna maji ya mvua na kuyatumia kwa kujenga mifumo ya uvunaji maji katika majengo yao. Pia Halmashauri imeazimia kila jingo la umma linalojengwa kuwepo mfumo wa kuvuna maji ya mvua.

7.4 MAENDELEO YA JAMII:

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma katika kutekeleza sera ya Maendeleo ya wanawake inalenga kusawazisha tofauti zilizopo baina ya wanawake na wanaume ili kuweka mazingira yatakayoweza wote kutekeleza majukumu yao katika kujitea maendeleo na kuondokana na umaskini kwa kuzingatia mahitaji ya kijinsia.

Katika kuzingatia umuhimu wa wanawake na mchango wao katika jamii Wilayani, zipo shughuli mbalimbali zilizotekelezwa ili kuhakikisha maendeleo ya wanawake na watoto yanapatikana ingawa pia bado kuna changamoto zinazopaswa kushughulikiwa ili kufanikisha maendeleo ya wanawake.

Baadhi ya shughuli zinazotekelezwa ni kama kama vile:-

- Kutoa mikopo ya riba nafuu kwa vikundi
Jumla ya vikundi vya vijana 51 vimepata mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 30 na jumla ya shilingi milioni 30 zimetolewa kwa vikundi vya akina mama vipatavyo 69 katika kata 16.
- Kutembelea asasi zisizojishughulisha na utunzaji wa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na yatima
- Kutoa mafunzo ya ujasiliamali kwa viongozi wa vikundi
- Kutoa elimu ya kujingika na maambukizi ya mapya Ukimwi katika jamii kwa njia ya sinema
- Kuwalipia karo wanafunzi 130 wanaosoma shule za sekondari, wanaoishi katika mazingira magumu kiasi cha sh.2,600,000/=
- Jumla sh. 6,000,000 zimetolewa kwa vikundi 12 vya wanaoishi na VVU.
- Kutambua na kutembelea asasi zisizo za kiserikali zilizopo ndani ya Manispaa ya Musoma.

TASAF III

Mpango huu unatekelezwa katika Kata 11 kati ya 16 za Manispaa ya Musoma na katika Mitaa 30 kati ya 73 iliyopo. Jumla ya kaya 3303 zimehakikiwa na kusajiliwa kati ya kaya 3493 zilizokuwa zimetambulishwa

Jedwali Na. 1: Hali ya utekelezaji wa TASAF awamu ya tatu

Utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (2013-2017)									
Mwaka 2013/2014					Mwaka 2014/2015				
Idadi ya Tarafa	Idadi Kata	Idadi ya Mitaa	Idadi ya Kaya	Miradi iliyo/inayotekelezwa	Idadi ya Tarafa	Idadi Kata	Idadi ya Mitaa	Idadi ya Kaya	Miradi iliyo/inayotekelezwa
0	0	0	0	0	1	13	57	4,063	Utoaji wa ruzuku kwenye kaya maskini

8.0 MWENENDO WA MAKUSANYO YA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Mapato ya ndani yamekuwa yakiongezeka baada ya Halmashauri kuchukua hatua mbalimbali katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato yake ya ndani. Hatua hizo ni pamoja na:-

- Kutoa matangazo sehemu mbalimbali kuhamasisha wafanya biashara kulipa ada za leseni kwa mujibu wa sheria.
- Kuunda timu ya ufuatiliaji mapato kwa kila chanzo.
- Kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wote wanaofanya biashara na Halmashauri wanalipa ushuru wa huduma kila malipo yanapofanyika na ufuatiliaji kwa wafanyabishara wengine kwa mujibu wa sheria unafanyika
- Kuimarisha takwimu za walipa kodi ili kuziba mianya ya wakwepa kodi
- Wadau mbalimbali wakiwemo viongozi na watendaji wa Halmashauri kuendelea kutoa elimu kwa walipa kodi.

Jedwali Na. 1: Mwenendo wa makusanyo ya ndani kuanzia mwaka 2012/2013 umeoneshwa katika jedwali lifuatalo:-

CHANZO CHA MAPATO	2012/2013		2013/2014		2014/15	HALISI HADI MAY. 15	% ANN UAL
	MAKISIO	HALISI	MAKISIO	HALISI	MAKISIO		
Kodi ya Majengo	95,626,100	75,284,205	123,592,822	84,297,388	140,617,000	54,902,415.00	39.04
Kodi ya Viwanja	12,153,600	31,864,500	18,230,400	18,710,892	81,000,000	39,096,582.00	48.27
Ushuru wa Huduma	187,681,230	188,538,887	210,133,230	204,275,241	234,102,000	228,091,812.42	97.43
Leseni za Biashara	330,000,000	2,704,800	330,635,000	135,108,124	357,995,000	215,950,872.00	60.32
Leseni za Pombe za Kigeni	17,260,000	10,394,500	9,380,000	16,151,400	10,548,000	7,960,000.00	75.46
Ushuru nyumba za kulala wageni	66,000,000	72,000,000	72,000,000	0	72,000,000	0	0
Ushuru wa Bus Stand na Taxi	97,380,000	70,191,100	97,380,000	102,276,000	110,000,000	94,490,000.00	85.90
Ushuru wa Maegesho ya magari	15,000,000	23,800,000	25,200,000	30,480,000	28,776,000	34,550,000.00	120.07
Ushuru wa Masoko/ Gulio fee	26,748,000	6,602,300	8,640,000	9,695,000	8,640,000	10,670,000.00	123.50
Ada ya maombi ya Tenda	7,200,000	8,007,000	7,200,000	5,747,283	9,400,000	7,910,000.00	84.15
Leseni za uvuvi	0		14,782,000	3,921,000	14,783,000	11,532,500.00	78.01
Ada ya matangazo na vibao	9,510,000	5,057,200	11,430,000	8,167,114	100,000,000	26,497,400.00	26.50
Ushuru wa Machinjio	19,267,000	6,949,150	17,712,000	14,132,600	40,500,000	41,154,900.00	101.62
Ushuru wa samaki na dagaa	728,000	18,509,867	36,000,000	6,866,100	42,600,000	44,550,000.00	104.58
Ada ya Usajili wa Taxi	0	0	1,940,000	1,770,000	1,975,000	100,000.00	5.06
Kodi ya vibanda vya Biashara	128,954,000	204,610,064	285,140,000	98,119,847	348,886,000	173,633,750.00	49.77
Kodi ya nyumba za H/mashauri	360,000	301,839	360,000	326,890	141,132	35,283.00	25
Tiba kwa kadi na papo kwa papo	0	0	0	0	137,500,000	70,778,509.00	51.48
Karo Shule za sekondari	0	0	0	0	321,960,000	206,051,814.47	64.00
Mapato mengineyo	12,000,000	18,351,560	12,000,000	11,601,050	20,000,000	12,286,250.00	61.43
Ushuru toka Bima	200,000	189,613	200,000	193,694	0	0	0
Bima ya Afya	20,025,000	6,489,053	0	0	0	0	0
JUMLA YA MAPATO YA NDANI	704,520,000	670,667,206	872,916,000	459,816,087	2,081,423,132	1,272,282,087.89	61.12

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Aidha Halmashauri ya Manispaa imekuwa ikipokea ruzuku toka Serikali Kuu ikiwa ni mishahara, matumizi mengineyo na miradi ya maendelo kama majedwali yafuatayo yanavyoonesha:-

Jedwali Na. 2: Ruzuku toka Serikali Kuu

MWAKA 2012/2013		MWAKA 2013/2014		MWAKA 2014/2015	
MISHAHARA	MATUMIZI MENGINE	MISHAHARA	MATUMIZI MENGINE	MISHAHARA	MATUMIZI MENGINE
10,515,907,903.19	2,265,400,663	11,588,757,832	1,993,751,500	6,966,905,996.54	731,032,847

Jedwali Na. 3: Ruzuku toka Serikali Kuu (Jumla Oct Mishahara + Miradi)

2011/2012	2012/2013	2013/2014	2014/2015
14,673,429,402	15,480,358,020	14,755,167,784.87	9,445,911,051.36

Jedwali Na. 4: Fedha zilizotengwa mwaka 2014/2015 kwa miradi ya maendeleo kwa Halmashauri kwa sekta za kipaumbele na Fedha za LGCDG

LGCDG	ELIMU (Local & Basket)	AFYA	HIV/AIDS PROJECT (TMAP*)	MAJI (Rural Water Supply & Sanitation - ADF)	KILIMO (ASDP Basket)	BARABARA (Mfuko wa barabara)
728,960,000	223,656,000	219,892,000	270,063,000	19,161,000	60,145,000	749,020,000

9.0. UDHIBITI WA MATUMIZI YA FEDHA ZA SERIKALI

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Halmashauri yake ya Manispaa ya Musoma imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kuwa udhibiti wa matumizi ya fedha za serikali unaimarika ambapo kwa sasa hali ni ya kuridhisha kama inavyooneshwa katika ripoti ya Udhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) kwenye jedwali linalofuata:-

Jedwali Na. 5: Mwenendo wa Hati yaukaguzi wa fedha za miradi katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma tangu kuanzia 2008/2009 – 2012/2013

AINA YA HATI					
2008/2009	2009/2010	2010/2011	2011/2012	2012/2013	2013/2014
Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

10.0. UTATUZI WA KERO MBALIMBALI ZA WANANCHI

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma inalo dawati la malalamiko linaloshughulikia kero mbalimbali za wananchi. Dawati la malalamiko limeanzishwa katika ngazi zote za utawala kwa maana ya Mitaa na Kata.

Kupitia dawati la malalamiko, kero mbalimbali za wananchi zimeshughulikiwa na kupata ufumbuzi mathalani kwa mwaka huu wa 2014 jumla ya malalamiko

73 yamesajiriwa katika rejesta ya malalamiko na tayari malalamiko 12 yamepatiwa ufumbuzi na malalamiko 61 yako katika hatua mbalimbali za utatuzi.

Aidha malalamiko/kero nyingi zinazopokelewa na dawati la malalamiko zinahusu masuala ya ardhi na uharibifu wa mazingira.

Manispaa ya Musoma inaunga mkono jitihada za serikali katika kushughulikia kero za wananchi kwa kutekeleza kwa vitendo Mwongozo wa kitaifa wa kuunda, kusimamia na kuendesha ofisi za malalamiko. Aidha utatuzi wa kero za wananchi unakwenda sambamba na utoaji wa elimu kwa wananchi na kuwepo kwa mkataba wa huduma kwa mteja, mkataba unatoa fursa kwa wananchi kufahamu wajibu na haki zao katika utumiaji wa huduma zitolewazo na Serikali kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.

11.0 UHUSIANO WA HALMASHAURI YA MANISPAA NA SERIKALI KUU

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Uhusiano kati ya Halmashauri ya Manispaa na Serikali Kuu kwa sasa siyo wa kuridhisha. Kuna kutoelewana kati ya Mhe. Mkuu wa Wilaya na baadhi ya Wahe. Madiwani. Kumejitokeza kauli za kupingana hasa kuhusu suala la Wananchi kuchangia Ujenzi wa Maabara na shughuli nyingine za maendeleo.

Tunakushukuru kwa hatua ulizoanza kuzichukua katika kuimarisha uongozi wa pamoja katika Wilaya yetu.

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Viongozi na wananchi wa Wilaya ya Musoma tunakushukuru sana kwa heshima uliyotupa ya kututembelea na tunakutakia ziara njema ya Wilaya ya Manispaa ya Musoma. Tuko tayari kupokea na kutekeleza maagizo, ushauri utakotoa wakati wote wa ziara yako.

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Kwa heshima na taadhima naomba kuwasilisha.

Mhe. Zelothe Stephen.
**MKUU WA WILAYA
MUSOMA**